

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Email –ded@kyeladc.go.tz
 Simu Na. 025-2540035/7
 Nukushi. 025-2540425



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
 S.L.P. 320, Kyela
MBEYA - TANZANIA

Tarehe 08/09/2018

Mh.Mwenyekiti
 Kamati ya
KYELA

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHO ISHIA 31 JULAI, 2018.

1.0 MUHTASARI WA MAPATO

Mh. Mwenyekiti, Halmashauri kwa Mwaka 2018/2019 imekisia kukusanya na kupokea jumla ya **Tshs 40,040,781,017** kutokana na vyanzo mbalimbali vya ndani, Ruzuku toka Serikali kuu ya Matumizi ya kawaida, Ruzuku ya Mishahara, Ruzuku ya Miradi (LOCAL) na Ruzuku ya wahisani Kwa mchanganuo ufuatao:-

| NA | | | | KIASI |
|----|--|------|----------------|-----------------------|
| 1 | VYANZO MBALIMBALI VYA HALMASHAURI/FIDIA | | | |
| | Vyanzo vya ndani | Tshs | 3,426,063,788 | |
| | Vyanzo vya ndani Mamlaka | Tshs | 534,945,000 | |
| | JUMLA NDOGO | | | 3,961,008,788 |
| 2 | RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU- | | | |
| | Mishahara | Tshs | 29,915,978,000 | |
| | Matumizi mengineyo | Tshs | 1,545,405,120 | |
| | Fidia ya Halmashauri | Tshs | 139,742,976 | |
| | JUMLA NDOGO | | | 31,601,126,096 |
| 3 | Miradi ya Maendeleo - Serikali Kuu (Local) | Tshs | | 1,460,427,500 |
| 4 | Miradi ya Maendeleo ya Wahisani (Wafadhili) | Tshs | | 3,018,218,611 |
| | JUMLA KUU | | | 40,040,781,017 |

Hadi 31 JULAI, 2018, Halmashauri imepokea na kukusanya jumla ya TSH **2,142,082,441** sawa na asilimia **5.34** ya makisio ya Tshs **40,040,781,017** kwa mwaka. Mapato hayo yamekusanywa na kupokelewa katika vyanzo vifuatavyo:-

| NA | Mchanganuo wa Mapato kwa muhtasari | | KIASI |
|----|--|------|----------------------|
| 1 | VYANZO MBALIMBALI VYA HALMASHAURI | | |
| | Vyanzo vya ndani vya Halmashauri | Tshs | 55,658,563 |
| | Vyanzo vya ndani Mamlaka | Tshs | 56,426,250 |
| | JUMLA NDOGO | | 112,084,813 |
| 2 | RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU- | | |
| | Mishahara | Tshs | 1,850,450,500 |
| | Matumizi mengineyo (OC) | Tshs | 0 |
| | Fidia ya vitengo | Tshs | 0 |
| | JUMLA NDOGO | | 1,850,450,500 |
| 3 | Miradi ya Maendeleo - Serikali Kuu (Local) | Tshs | 113,820,581 |
| 4 | Miradi ya Maendeleo na Wahisani -(Foreign) | Tshs | 177,811,360 |
| | | | 291,631,941 |
| . | JUMLA KUU | | 2,142,082,441 |

Hadi **31 JULAI 2018** vyanzo vya ndani vya Halmashauri vimekusanya jumla ya Tshs. **112,084,813** sawa na asilimia **2.83%** ikilinganishwa na matarajio ya kukusanya asilimia 8.3% hadi **JULAI 31, 2018** ya makisio ya Tshs **3,961,008,788** kwa mwaka 2018/2019 ikiwa na upungufu wa asilimia **5** ya lengo lililotarajiwa. Kwa mwezi **JULAI** pekee kiasi cha Tshs **112,084,813** kimekusanywa ambapo Mamlaka ya Mji Mdogo imekusanya Tsh.**56,426,250** na Halmashauri Tsh.**55,658,563**

MATUMIZI

Makisio kwa mwaka 2018/2019 ni jumla ya Tshs **40,040,781,017** hadi kufikia tarehe **31 JULAI, 2018** Halmashauri imetumia jumla ya **1,964,271,081** sawa na asilimia **4.91%** ya makisio kwa mwaka.kwa mchanganuo ufuatao:

| | MCHANGANUO WA MATUMIZI KWA MUHTASARI | KIASI |
|---|---|----------------------|
| 1 | Matumizi ya kawaida vyanzo vya ndani Tshs 0 Matumizi yatokanayo na vyanzo vya Miradi ya maendeleo(own source dev)Tshs 0 | 0 |
| 2 | RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU- Mishahara Tshs 1,850,450,500 Matumizi mengineyo (OC) Tshs 0 Fidia ya vitengo Tshs 0 JUMLA | 1,850,450,500 |
| 3 | Miradi ya Maendeleo - Serikali Kuu (Local) Tshs 113,820,581 | |
| 4 | Miradi ya Maendeleo na Wahisani -(Foreign) Tshs 0 | 113,820,581 |
| | JUMLA | 1,964,271,081 |

2.0. MCHANGANUO WA MATUMIZI

2.1.VYANZO VYA NDANI VYA HALMASHAURI

Makisio ya matumizi ya vyanzo vya ndani kwa mwaka ni Tshs **3,961,008,788.00**. Hadi kufikia tarehe 31 JULAI, 2018 zimetumika jumla ya Tshs **0** sawa na asilimia **0%** ya makisio kwa mwaka. Kwa mwezi JULAI pekee zimetumika **Tsh. 0** sawa na asilimia **0%** ya makisio kwa mwaka.

2.2.RUZUKU YA KUENDESHA OFISI

Ruzuku ya kuendesha ofisi na Mishahara ina makisio ya Tshs. **31,601,126,064** na hadi kufikia **31 JULAI ,2018** zimetumika Tsh **1,850,450,500** sawa na asilimia **6%** ya makisio kwa mwaka. Kwa mwezi **Julai** pekee zimetumika Tshs.**1850,450,500** sawa na asilimia **6%** ya makisio kwa mwaka.

2.3. RUZUKU YA MAENDELEO TOKA SERIKALI KUU (LOCAL)

Makisio ya matumizi ya miradi ya Ruzuku toka serikali kuu, kwa mwaka 2018/2019 ni Shs.**1,460,427500** hadi kufikia **31 JULAI, 2018** , kiasi cha Tshs **113,820,581** zimetumika sawa na asilimia **8%** ya makisio kwa mwaka.

2.4. MATUMIZI YA MIRADI – WAHISANI

Makisio ya matumizi fedha za miradi toka kwa Wahisani kwa mwaka 2018/2019 ni Shs **3,018,218,611** na hadi kufikia tarehe **31 JULAI 2018** , kiasi cha **Tshs 0** zilitumika sawa na asilimia **0%** ya makisio kwa mwaka

2.5. BAKAA YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

Bakaa ya fedha kwa mwaka 2017/2018 ni Tsh. **1,254,703,398.23** kama inavyoonekana kwenye jedwali

| | |
|----------------------|-------------------------|
| AKAUNTI YA MAENDELEO | 16,787,238.26 |
| AKAUNTI YA ELIMU | 27,198,099.49 |
| AKAUNTI YA AFYA | 428,400,057.34 |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 8,783,522.52 |
| MFUKO WA BARABARA | 465,148,011.61 |
| AKAUNTI YA MAJI | 204,767,331.15 |
| AKAUNTI YA AMANA | 54,682,255.47 |
| AKAUNTI YA MISHAHARA | 27,804,235.47 |
| MFUKO MKUU | 21,132,646.92 |
| JUMLA | 1,254,703,398.23 |

Hadi kufikia **31,JULAI,2018** Hakukuwa na Matumizi yoyote ya Bakaa.

CHANGAMOTO ZILIZOJITokeza UKUSANYAJI MAPATO 2018/2019.

- Ushuru wa Kokoa ambao ndio chanzo kikubwa bado haukusanyiki ipasavyo kufuatia agizo la Serikali la kuanzisha Ushirika badala ya Makampuni binafsi hata hivyo bei elekezi ya kokoa imeshuka toka Tsh.4,200 kwa kilo hadi Sh.3,550.
- Watendaji wa vijiji kutowajibika vizuri katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo yao ya kazi na hivyo kupoteza mapato.

MIKAKATI ILIYOPO KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO

- Kuimarisha mageti yanayotoka nje ya wilaya na kuweka vijana kwa mikataba ambao watafanya kazi siku nzima (Masaa 24) kwenye vituo husika.
- Kuendelea kufuatilia minada yote ya kokoa kila inapofanyika.
- Mkataba umeandaliwa na baada ya kupitishwa kwenye vikao matangazo na vigezo vya kuwapata vijana yatapelekwa vijijini ili watafutwe kwa kila kijiji.
- Wakuu wa Idara kutoka na kufuatilia mapato vijijini.

P.G.Msafi
Kny.Mkurugenzi Mtendaji(W).
Kyela.